# FRONTRUNNER EXAM

## DARASA LA NANE 2021 ⟨8⟩

## KISWAHILI

FRONTRUNNER 007

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa jibu lifaalo zaidi.***

Kuzorota kwa hali ya usalama __1__ mataifa mengi __2__ jambo linalowasumbua viongozi wengi. Wengi wao wanaambulia usingizi wa __3__ kutokana na jinamizi __4__. Iwapo mikakati kabambe haitawekwa ili __5__ hali hii, basi __6__ uchumi wa nchi nyingi ukaanza __7__. Tatizo lenyewe halina budi kuvaliwa njuga kabla ya mambo kuenda __8,__ kwani wahenga walisema __9__.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ya | katika | kwa | na |
| 2. | limekuwa | yamekuwa | kumekuwa | umekuwa |
| 3. | mang'amung'amu | pono | mwanana | mbaya |
| 4. | hizi | huu | hii | hili |
| 5. | kuikabili | kuikabidhi | kukabiliwa | kukabidhiwa |
| 6. | huja | huenda | pengine | labda |
| 7. | kuimarika | kuibuka | kudidimia | kukua |
| 8. | mserego | joshi | shoti | mrama |
| 9. | usipoziba ufa utajenga ukuta | dau la mnyonge haliendi joshi | aliye kando haangukiwi na mti | msafiri ni aliye pwani |

Mawasiliano __10__ hatua kubwa __11__ miaka ya tisini. Vyombo mbalimbali vimevumbuliwa vikiwemo __12__. __13__ yake ni kuwa habari muhimu zimeweza kuifikia __14__ lengwa kwa urahisi na upesi sana. Hata hivyo, hakuna masika yasiyokuwa na mbu. Vyombo __15__ vimeweza pia kutumiwa kueneza uvumi na kuwatenganisha watu.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 10. | yamepiga | imepiga | zimechukua | yamechukua |
| 11. | mpaka | tangu | hadi | lau |
| 12. | rununu, nukulishi na kambarau | redio, televisheni na jirafu | jarida, tarakilishi na eleveta | rungoya, runinga na rukono |
| 13. | Uzuri | Maana | Matokeo | Hasara |
| 14. | hadhira | hadhari | adinasi | hadhiri |
| 15. | hivyo vivyo | zizi hizi | hivi vivi | vivi hivi |

***Kuanzia nambari 16 - 30, jibu kila swali kulingana na maagizo.***

16. Kamilisha kwa ufasaha kwa kuzingatia msamiati wa mahakama
Baada ya kusomewa hukumu yake aliamua ______ kupitia kwa wakili wake.
A. kuruka kesi B. kuweka dhamana
C. kukata rufaa D. kukiri mashtaka

17. Ni sentensi gani iliyotumia **katika** kuonyesha shughuli fulani?
A. Panya alijificha katika shimo hili
B. Kiswahili hutumika sana katika biashara
C. Kamba haiwezi kukatika kwa gamba
D. Samaki huishi katika maji

18. Tambulisha sentensi yenye kielezi kikariri.
A. Maneno yake yalinikereza kama msumeno
B. Kazi ikifanywa haraka haraka itavurugika
C. Ukikosa heshima utaadhibiwa kimotoni
D. Mtoto wake ni mtiifu kuliko huyu

19. Neno **'anayempiga'** lina viambishi vingapi?
A. Vitatu B. Vinne
C. Sita D. Vitano

20. Jozi ipi inaonyesha kitenzi kilichoundwa kutokana na nomino?
A. Uchovu -choka B. Vumilivu - vumilia
C. Msikivu - usikivu D. Mbio - mkimbizi

21. Maelezo yapi ni sahihi kuhusu uakifishaji?
A. Nukta mkato hutumiwa kutanguliza orodha.
B. Alama hisi inaweza kutumika kuulizia swali.
C. Koloni hutumiwa kutanguliza wahusika wa tamthilia.
D. Kiulizi huonyesha hisia za mnenaji.

22. "Ukitaka kula nguruwe chagua aliyenona".
Methali hii hutumiwa kutufahamisha kuwa
A. dhambi ni dhambi, iwe kubwa au ndogo
B. ukiamua kutenda wema usingoje kulipwa
C. utendapo jambo zuri jitolee kikamilifu
D. amtegemeaye tajiri au mjuzi hufaidika

23. Bainisha sentensi yenye **nomino ya kawaida.**
A. Mate yalimdondoka ndo-ndo-ndo.
B. Seremala aliziunda meza nzuri.
C. Ulezi mwema ulimfunza maadili.
D. Waliiona thurea ya nyota usiku.

24. Chagua maelezo yaliyo sahihi
A. Masizi ni uchafu wa moshi unaoninginia darini.
B. Kifumbu hutumika kufunikia chungu jikoni.
C. Utando ni wali ulioungua chini ya sufuria.
D. Legeni hutumiwa kuokea mikate ya kumimina.

25. Sentensi ipi imetumia kiulizi kifaacho zaidi?
A. Vigoda vigani vitakaliwa na wazee?
B. Vigoda gani vitakaliwa na wazee?
C. Vigoda ngapi vitakaliwa na wazee?
D. Vigoda zipi zitakaliwa na wazee?

26. Kanusha: ***Nilipomwona alikuwa akisuka mikeka.***
A. Nilipomwona alikuwa hasuki mikeka.
B. Sikumwona wala hakuwa akisuka mikeka
C. Nilipomwona hakuwa akisuka mikeka
D. Nisipomwona hakuwa akisuka mikeka

27. Kiwakilishi kionyeshi kinapatikana kwenye sentensi gani?
A. Haya yananukia kuliko yale.
B. Vyenu ni vizuri kuliko vyao.
C. Lolote utakaloomba litatimizwa.
D. Ambamo amejificha mna giza jingi.

28. Tumia kiunganishi kifaacho zaidi kukamilishia sentensi ifuatayo:
Nyumba za huku ni za aushi, ______ huwa za mawe.
A. ilhali B. almuradi
C. aghalabu D. alaakulihali

29. Sungura kwa kitungule ni mithili ya bata kwa ______
A. kidue B. kivinimbi
C. kimatu D. kiyoyo

30. Tegua kitendawili: Askari wanapigana huku wakiunguzwa.
A. bisi B. kuni
C. chungu D. umeme

***<u>Yasome makala haya kisha ujibu maswali</u>* 31 – 40**

Utawala bora huhusisha mambo kadha wa kadha. Sheria zinazoheshimu maisha ya binadamu ni nguzo muhimu katika kufanikisha utawala wowote ule. Kuheshimu dini za raia pia huchangia sana katika kufaulisha utawala. Watu wana imani kuhusu Mungu wao na ni heshima kubwa iwapo utawala wao utaipa imani yao mbolea ya kukua.

Taifa lolote duniani likiwa limekosa elimu kwa watu wake ni taifa lisilo na maendeleo. Elimu ni ufunguo katika kufikia maendeleo mengi na sahihi. Kiongozi mwema anafaa azingatie wazo hili na kujitahidi kulitekeleza.

Kiumbe yeyote akikosa **siha** njema huathirika vibaya mno katika maisha. Unyonge wa kiumbe unaosababishwa na siha duni hufanya kiumbe huyo kuwategemea wenzake **walio wazima**. Siha bora ni nguzo muhimu katika ufanisi wa nchi na hivyo basi utawala bora hauna budi kutoa huduma za afya kwa raia wake. Iwapo jambo hili litafaulu, serikali husika ni bora itoze malipo ambayo raia wake watamudu kugharamia kwa njia rahisi.

Uwazi na uwajibikaji ni sera nzuri inayofaa kuandamwa na utawala wowote ulio mwema. Mtu aweze kuhudumiwa pasipo uwezo wa ukabila, dini, elimu na mengine mengi ambayo hukwaza utawala bora. Ufisadi na ubinafsi aidha ukipigwa vita miongoni mwa wanajamii, jamii husika itatajika kama jamii iliyo na utawala bora.

Utawala bora huimarisha usawa wa raia wake kwa kugawa rasilimali za nchi bila mapendeleo na kusambaza huduma zake kote nchini kulingana na mahitaji ya maeneo mbalimbali. Licha ya hayo, ni vyema kiongozi bora kuhimiza udumishaji historia na tamaduni za watu wake. Hili linapofanyika utaifa hukuzwa na kuheshimiwa. Historia hii na tamaduni hizo zaweza kuhifadhiwa katika maandishi au masimulizi kupitia sherehe za kitaifa, yamkini mara moja katika mwaka.

Mashujaa wa nchi wanapokumbukwa na kuheshimiwa huashiria utawala ulio mzuri. Mashujaa hawa wanaweza kuwa wa kisiasa, kielimu, sayansi na teknolojia, michezo au hata magwiji wa kuhifadhi historia ya nchi. Maeneo mbalimbali yanaweza kupatiwa majina yao au hata pengine waweze kujengewa minara ya ukumbusho.

Hapana nchi iwezayo kujiendeleza yenyewe pasi na uhusiano mwema na majirani zake na ulimwengu kwa jumla. Utawala mwema basi ni ule unaopalilia jambo hili na kupiga vita vikwazo vyovyote ambavyo vitakwaza azma hii.

31. Kulingana na aya ya kwanza, utawala bora hufaulishwa na yote haya ila
A. sheria zinazotukuza maisha ya binadamu
B. kumwagia imani ya watu mbolea nzuri
C. kuepuka sheria zinazokandamiza maisha
D. kuheshimu imani za watu mbalimbali.

32. Umuhimu wa elimu katika kufanikisha maendeleo ni kuwa
A. watu wote waliosoma hupata ajira nzuri
B. watu wenye elimu hupata sifa nzuri kimataifa
C. watu waliosoma hawawezi kuzivunja sheria za nchi
D. watu waliosoma huinua nyanja mbalimbali nchini.

33. Neno **'siha'** kama lilivyotumika katika makala ni kisawe cha neno
A. rai B. sifa C. nguvu D. sihi

34. Watu walio wazima kulingana na muktadha ni
A. wenye umri mkubwa
B. wale ambao si watoto
C. wasio na matatizo ya kiafya
D. wenye akili timamu.

35. Mwandishi wa makala uliyoyasoma anapendekeza
A. huduma za afya ziwe za bwerere
B. huduma za afya ziwe za bei rafi
C. huduma za afya ziwe za bei nafuu
D. huduma za afya ziwe ghali.

36. Kuwahudumia watu kulingana na kabila, dini au elimu kwa jumla ni
A. ubaguzi B. ufisadi C. ubinafsi D. uadilifu.

37. Njia mwafaka zaidi ya kuimarisha usawa ni
A. kusawazisha huduma zinazotolewa katika maeneo yote
B. kutoa huduma kulingana na mahitaji ya kila eneo
C. kupeleka huduma zote katika maeneo yaliyobaki nyuma.
D. kuacha kila eneo lijisimamie kwa rasilimali zake.

38. Mwandishi anasema kuwa utaifa hukuzwa kwa
A. kuanzisha historia na utamaduni
B. kuiga tamaduni za nchi zilizostawi
C. kujiepusha na lolote litokalo nje ya nchi
D. kudumisha historia na utamaduni

39. Maeneo na minara hupewa majina ya mashujaa ili
A. waheshimiwe, wasisahaulike na waigwe
B. wapendewe, wasisahaulike na waigwe
C. waonekane, waigwe na wasisahaulike
D. wapendwe, waheshimiwe na waonekane.

40. Kichwa mwafaka kwa makala haya ni:
A. Uhusiano mwema wa raia na viongozi
B. Umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa
C. Nguzo za kuimarisha utawala bora
D. Umuhimu wa elimu, dini na utawala.

***<u>Soma kisa kifuatacho kisha ujibu maswali</u>* <u>41 – 50</u>**

Mlapa aliendelea kuzama kwenye hekaheka za mji. Asubuhi aliamkia gange yake ya kusukuma rukwama. Kazi hii aliifanya kutwa, katika masoko na vichochoro vya mji akiwabebea watu bidhaa kwa malipo duni. Pesa alizozipata ndizo zilizomwezesha kuumudu ulevi wake wa pombe hatari, kulipia chumba kimoja alichokodi kwenye mtaa wa mabanda, na kugharamia chakula chake; ambacho bila shaka unaweza kutabiri hali yake. Kila jioni alijiunga na watu kufu yake kushiriki ugimbi na starehe nyingine ambazo wangemudu.

Mara nyingi Mlapa na waraibu wenzake, walijipata wameangukia kwenye mikwaruzo ya walinda usalama, wakasombwa kama taka na kutiwa kwenye malori yaliyowapeleka kwenye seli mbalimbali. Hapo walioweza kutoa **kinyegezi** wangefanya hivyo na kuachiliwa. Ole wao ambao walijitia kuchanikiwa na vibindo. Wangerambishwa mateke ya kila aina na kufundikwa ndani hadi wakati wangepata msamaria mwema wa kuja kuwatoa humo kwa dhamana ambayo iliishia mikononi mwa walinda haki na vituo vya polisi.

Hali iliendelea kumwia ngumu Mlapa katika mji huu wa watu. Hakuwa ameyazoea maisha haya ya kuchanika kwenye mpini kila mara na kufa njaa wakati huo huo. Aliishi na wenzake ambao tayari walikuwa wamevizoea vitimbi vya mji. Wao waliumudu ulevi kila siku na kupata pesa za kuwapenyezea wenye macho mapekuzi. Hata hivyo, hali ya Mlapa haikuwa ya kuridhisha. Dhoruba za mji zilimpiga yeye maradufu ya vijana wenzake. Hawakusema wasemao kuwa baridi humzizima kondoo mwenye manyoya haba? Mlapa alikuwa mwanagenzi katika maisha ya mji na daima mwanagenzi huwa na mengi ya kujutia.

Ijumaa moja usiku wa manane, Mlapa aliamshwa na vishindo vya watu na sauti za magari. Alichungulia kwenye tundu aliloita dirisha la chumba chake na kukumbana na mianga mikali ya matingatinga yaliyokuwa yakijiendea tu bila kujali kuwa yalikuwa yakipitia juu ya nyumba za wachochole hawa.

Mlapa aliangalia kwa jitimai ya kudhalilisha nafsi vibanda vya majirani vikinywea na kuanguka chini kutokana na shinikizo la msema kweli huyu. Alimaizi kuwa wakati wa kuokoa kidogo alichokuwa nacho ulikuwa umewadia. Alijizoazoa na kuanza kukusanya milki ya pekee aliyokuwa nayo. Hata kabla ya kuchukua chochote, alisikia sauti kali ikimwambia **atoke kabla hajawa kima**. Mlapa akatii amri, akachukua furushi lililojaa magwanda yake ya kazi na kutoka. Tingatinga halikuchelewa kukilainisha kibanda chake na kumkumbusha kuwa maisha yake na wenzake yalikuwa yamechukua mkondo mpya.

Upepo yabisi wa alfajiri ulimpata Mlapa amejishika tama mbele ya kilichokuwa kibanda chake. Hakujua kwa nini alikuwa kaandamwa na nuksi ya aina hii. Alipowauliza wenzake kisa na maana ya haya, aliambiwa kuwa hiyo ilikuwa shughuli ya kidesturi ya serikali kuusafisha mji na kupunguza ombaomba katika ?aa iliyopakana na mitaa ya kifahari. Ingawa Mlapa alikuwa kakatika maini, wenzake hawakuonekana kupigwa na mshipa. Walisema wangengoja siku mbili tatu chura hawa wasahau kisha warudi kuvijenga upya vibanda vyao. Mlapa alijiona kama nyumba ya udongo isiyoweza kuhimili vishindo. Moyo wake ulimuasa kuwa yeye **alikuwa jogoo la shamba na tangu hapo jogoo la shamba haliwiki mjini**. Aliamua kufunganya virago vyake na kurudi nyumbani kuanza maisha upya.

**41.** Chagua kauli sahihi kwa mujibu wa makala
- A. Mlapa alikuwa mzegazega
- B. Mlapa alikuwa hamali
- C. Mlapa alikuwa dereva
- D. Mlapa alikuwa kuli.

**42.** Uraibu wake Mlapa ulikuwa
- A. wa pombe haramu
- B. wa kutafuna miraa
- C. wa kula vyakula duni
- D. wa maisha ya uchochole

**43.** Walioungana na Mlapa jioni aghalabu walikuwa
- A. vijana wa hirimu yake
- B watu wa kila tabaka
- C. wahuni wa pale mjini
- D. walalahoi wenzake.

**44.** '**Kinyegezi**' kulingana na makala haya ni
- A. kombozi
- B. faini
- C. dhamana
- D. mlungula

**45.** Tatizo kuu alilokabiliana nalo Mlapa lilikuwa ni
- A. kutozoea kujifanyia lolote katika maisha yake
- B. kukabiliana na walinda usalama mara kwa mara
- C. kufanya bidii sana na kupata ujira duni
- D. kubugia ugimbi bila kula chakula cha kutosha

**46.** Ama kusema kweli
- A. Mlapa aliteseka mithili ya wenzake mjini
- B. Mlapa aliteseka kuliko wenzake mjini
- C. wenzake Mlapa hawakuteseka mjini
- D. Mateso ya akina Mlapa yaliletwa na serikali.

**47.** Vibanda vya Mlapa na wenzake vilibomolewa maadamu
- A. vilionekana duni karibu na makao ya mabwanyenye
- B. havikufaa kwa binadamu wowote kuishi mle
- C. vilijengwa katika eneo lililokuwa mali ya serikali
- D. vilijengwa katika milki ya mtu binafsi.

**48.** Maana ya '**atoke kabla hajawa kima**' ni
- A. aondoke kabla hajawa kama nyani
- B. atoroke kabla ya kuangukiwa na kibanda
- C. ajinusuru kabla ya kusagwa na tingatinga
- D. akimbie kabla ya kunaswa na askari.

**49.** Wenzake Mlapa hawakuwa na hofu kwa kuwa
- A. walikuwa wameinusuru mali yao
- B. hali kama hii ilikuwa kawaida kwao
- C. serikali iliahidi kuwalipa fidia
- D. wangejengewa vibanda upya baada ya muda.

**50.** **"......alikuwa jogoo la shamba na tangu hapo jogoo la shamba haliwiki mjini"** Kifungu hiki kinaonyesha
- A. alikuwa amechoshwa na vituko vya mjini
- B. alikuwa ameshindwa kuzimudu raha za mji
- C. alianza kutamani kutorokea mashambani
- D. alishindwa kukabiliana na hali ya mjini.